# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## BARAZA LA MITIHANI
## MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

**663** **MISINGI YA ELIMU**

**Muda: Saa 3** **Jumatano 7 Mei 2008 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawilil (2)** kutoka sehemu B na swali **moja (1)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 36, sehemu B ina alama 40 na sehemu C ina alama 24.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (alama 36)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza umuhimu wa elimu linganishi.

2. Eleza maana ya falsafa ya elimu.

3. Taja matokeo **matatu (3)** muhimu ya kutaifisha shule baada ya Azimio la Arusha.

4. John Locke (1632 – 1704) alitoa mawazo gani kufuatana na utoaji wa elimu kwa watoto?

5. Taja taofauti kuu **nne (4)** kati ya mwanafunzi mtoto na mwanafunzi mtu mzima.

6. Unaelewa nini kuhusu mawakala wa Elimu ya Watu Wazima Tanzania?

7. Falsafa ya Maria Montessori (1870 – 1952) imejikita katika mambo makuu **mawili (2)** kuhusu elimu ya mtoto. Yataje.

8. Andika sababu **tatu (3)** zinazoweza kuathiri mahudhurio ya mwanafunzi mtu mzima anayehudhuria darasa la Kisomo Chenye Manufaa.

9. Taja majina kamili ya wanafalsafa **wawili (2)** walioshughulikia Elimu ya Watu Wazima.

## SEHEMU B (alama 40)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

10. Eleza sababu anuai za kuwepo kwa michepuo ya elimu nchini Tanzania.

11. Fafanua mambo ya msingi mwanafalsafa John Dewey (1859 – 1952) aliyosisitiza katika ufundishaji kutokana na uzoefu wake.

12. (a) Sosholojia ya elimu ni nini?

    (b) Eleza michango mbalimbali inayotolewa na mawakala wa sosholojia ya elimu katika kumlea mtoto.

13. Eleza mambo makuu **manne (4)** ya kijamii yanayoweza kuathiri elimu Tanzania.

## SEHEMU C (alama 24)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Jadili faida na mapungufu ya elimu ya jadi katika jamii ya Tanzania visiwani.

15. Elimu haina mwisho. Jadili dhana hiyo kwa kutumia mifano kutoka kwa wanafalsafa mbali mbali wa Elimu ya Watu Wazima.

16. Eleza mambo (matakwa) **manne (4)** utakayozingatia wakati wa kumfundisha mwanafunzi mtu mzima.

Kiakili
Kimaumbile
Kijamii
Kisaikolojia
Kimazingira

Kiakili
- Kushirikishwa
- Kutumia mbinu sahihi
- Uwezo wake wa akili

Kimaumbile
- Kuona
- Kusikia
- Ku

Kijamii
- Majukumu

Kimazingira
ya nje
ya ndani